**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI YA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI MVUTI**

**Anwani ya simu**
**Simu: +255 712 987860**
**OFISI YA MKUU WA SHULE.**
**KATA YA MSONGOLA.**

**S.L.P 69032.**
**DAR ES SALAAM,**
**TANZANIA**

Kumb. Na. MVT/SEK/F1/2026
**JINA LA MWANAFUNZI**
………………..........…………………………………..
…
S.L.P ..............................................................................
.........................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MVUTI HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2026.**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **KWANZA** kama mwanafunzi katika shule hii kwa mwaka 2026. Shule ya Sekondari **MVUTI** ipo kusini mwa Jiji la Dar es salaam.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **05.01.2026**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **05.01.2026** kwa ajili ya usajili.

## *2.0* MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### *2.1* Sare za Shule

*(a)* **Wavulana**

- Suruali 2 za linda rangi ya Blue Bahari,
- Mashati 2 meupe mikono mifupi
- Soksi nyeusi jozi (pea) mbili (2)
- Viatu vyeusi vya kamba
- Sweta la Shule rangi ya Blue Masai.
- **Maelezo ya mshono**
  **(***Suruali ndefu mzunguko wa chini 16 yenye 'turn up')*

*(b)* **Wasichana**

- Sketi 2 rangi ya Blue Bahari
- Mashati 2 meupe mikono mifupi kwa wakristo
- Nusu Kanzu na Majuba 2 meupe kwa waislamu.
- Soksi nyeupe fupi jozi 2
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2 (pair 2).
- Sweta la Shule rangi ya Blue Masai
- **Maelezo ya mshono**
  *(Sketi ndefu inayogusa unyayo wa mguu. Mshono wa sketi ni Linda box).*

***2.2*** **Kwa wanafunzi wa kutwa**

- Chakula cha mchana, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la Mzazi / mlezi.

## *3.0* Sheria na Kanuni Muhimu za Shule.

***3.1*** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

a.H eshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
a/. ahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
a0. ushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation) kwa wakati.
a1. uwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
a2. ufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
a3. utunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kama vile Chooni, Madarasani, Bwenini,
a4. uvaa sare ya shule kwa ukamilifu wakati wote wa shule.
a5. uzingatia ratiba ya shule wakati wote wa muhula wa Masomo.
a6. utunza mali za umma kama vile Samani, Miundombinu ya Umeme, Maji, na rangi za kuta za majengo.
a7. uhudhuria masomo kulingana na ratiba ya shule.

## *3.2* MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

i. Kuchelewa kufika / kuripoti shuleni siku ya kufungua / kuanza shule au baada ya kumalizika kwa likizo ndefu / fupi.
ii. Wizi.
iii. Uasherati, usagaji, ushoga na Ubakaji.

iv. Ulevi, uvutaji sigara na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga, na kuzua taharuki.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
viii. Kuoa, kuolewa, kusababisha mimba na kutoa mimba.
ix. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
x. Kukataa/kugoma adhabu kwa makusudi.
xi. Kuwa na simu ya mkononi, Flash, Earphone na Radio shuleni.

## *4.0* <u>VIFAA / VITU VYA MUHIMU VINAVYOHITAJIKA SHULENI</u>.

**A) MUHIMU KWA MZAZI / MLEZI.**

- **Kila mzazi ambaye atamleta mwanafunzi (**Bweni/Kutwa**) kusoma katika shule yetu, atatakiwa kuja na Meza / Kiti kwa ajili ya kukalia mwanafunzi / mwanao (***Mchoro na vipimo kama inavyoonekana***)**

**B) TAALUMA**

– Ream Paper 1 (*Bunda moja la karatasi nyeupe*) (*ambayo haijafunguliwa*)
– Counter Book 9 (QUIRE 2/3/4)
– Daftari za Msomi 09
– Mkebe/Compass / Ruler ndefu (sm30), Peni na Penseli.
– **File (*kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za kitaaluma*) – *shuleni***
**– Kitambulisho cha shule– *shuleni***
**– Nembo ya shule– *shuleni***
**– T-shirt Ya shule – *shuleni***

**C) VIFAA VYA USAFI (*Kwa Wanafunzi wa Kutwa*)**

- Ufagio Mrefu wa Chelewa (*Kufagilia uwanja*)
- Fagio la Ndani / Soft Broom (*Kufagilia darasani*)
- Kwanja /Fyekeo
- Squizzer (skwiza)

***4.1*** **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Kamati ya Mapokezi mara tu, utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ya Elimu Namba 25 ya Mwaka 1978 na kufanyiwa marejeo mwaka 2015.

c) Picha mbili (passport size) za wazazi/ walezi ( baba moja, mama moja)

d) Picha mbili (passport size ) za mwanafunzi.

***5.0*** Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**

............................................................

**GASPER ANTHONY MWAIPOPO**
**Mkuu Wa Shule Mvuti Sekondari**

**KIAMBATANISHO A**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**MVUTI SECONDARY SCHOOL**

PICHA YA
MWANAFUNZI

To be completed by a Government Medical Officer

To Medical Officer

…………………………………..
Date ……………………………

**NAME OF STUDENT:** ………………………………………………………………………………….

Please examine the person mentioned above and comment on his/her health responsible to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either YES or NO

Does the student has problems in connection with

*a)* Sight? ……………………………………………………………………………… 1. NO
2.YES
If yes, state………………………………………………………………………………
*b)* Hearing………………………………………………………………………………1.NO
2. YES
If yes, state………………………………………………………………………………
*c)* Speech …………………………………………………………………………….1. NO
2. YES
If yes, state………………………………………………………………………………
*d)* T.b? ………………………………………………………………………………1.NO
2. YES
If yes, state………………………………………………………………………………
*c)* Blood pressure ……………………………………………………………… 1. NO
2. YES
If yes, state………………………………………………………………………………

*d)* Any physical disability ………………………………………………………1. NO
2.YES
If yes, state…………………………………………………………………………………
*e)* Do you therefore, recommend the said student medically: in for studentship at this section?
*I.* Yes 2. No
If no please state…………………………………………………………………………

Date ……………………………. Name & Signature …………………………………...

Designation's stamp …………………………………………………

# KIAMBATANISHO KWA WANAFUNZI WA BWENINI

Uongozi wa shule unayofuraha kukutaarifu kwamba mwanao amepangiwa kukaa BWENI. Mzazi utawajibika kutimiza wajibu wako kwa kuzingatia maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari MVUTI, hii ni pamoja na matibabu ya mwanao, nauli ya kwenda nyumbani na kurudi shuleni wakati wa likizo na vifaa vyake vya kutumia awapo BWENI.

**MASHARTI:**

Uhitaji wa BWENI ni mkubwa hivyo mwanao hataendelea kuishi BWENI ifikapo mwisho wa mwaka endapo atashindwa kutimiza masharti ya BWENI na si mtoto tu hata wewe mzazi unaweza kusababisha mwanao asiendelee kuwepo BWENI na kuwapisha watoto wengine ambao wanauhitaji huo.

1. Atawajibika kupata ufaulu wa **daraja** la **KWANZA** hadi **daraja** la **TATU (DIVISION I, II & III)** ifikapo mwisho wa mwaka wa masomo. Wastani huu ni majumuisho ya mitihani na majaribio yote ya mwaka husika.
2. Mawasiliano yote kati ya Mzazi/Mlezi na mwanafunzi yatafanyika kupitia kwa Mkuu wa Shule/ Makamu Mkuu wa Shule / Patron / Matron au Mwalimu Mlezi wa BWENI.
3. Mzazi atawajibika kuacha mawasiliano ya simu ambayo itapatikana muda wote na hataruhusiwa kufika shuleni kuonana na mtoto isipokuwa siku maalum ya kumtembelea mwanafunzi itapangwa na uongozi wa shule na taarifa zitawafikia wazazi na walezi.
4. Mtoto atawajibika kufuata masharti na taratibu zote atakazopewa awapo **BWENI**.
5. Kila mzazi ni lazima ahakikishe kuwa mtoto amekatiwa **BIMA YA AFYA** kwa ajili ya matibabu.
6. Nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo ni Jukumu la Mzazi / Mlezi.

**VIFAA VYA BWENI KWA WASICHANA**

1. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
2. Ndoo (lita 10) na beseni kwa ajili ya kuogea na kufulia
3. Taulo, shuka mbili rangi ya PINKI, mto (pillow) yenye foronya ya PINKI, Chandarua rangi Nyeupe/Pinki, Godoro la futi tatu (3 kwa 6) n a Pasi ya mkaa
4. Shamba dress (*Kitambaa Kizito cha Rangi Ya Damu Ya Mzee (Maroon*))
5. Ufagio Mrefu wa Chelewa (*Kufagilia uwanja*
6. Brush ndogo za kusugulia sink (chooni).
7. Jembe 1 + mpini wake
8. Mopa na Ndoo yake
9. Hard broom (fagio gumu)

**VIFAA VYA BWENI KWA WAVULANA**

1) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
2) Ndoo *(lita 10*) na beseni kwa ajili ya kuogea na kufulia
3) Taulo, shuka mbili rangi ya BLUE, mto (pillow) wenye foronya ya BLUE, Chandarua rangi nyeupe/blue, Godoro la futi tatu (3x6) na Pasi ya mkaa.
4) Shamba dress (*Suruali Rangi Ya Maroun Damu Ya Mzee*) na Tshirt rangi ya NJANO yenye Nembo ya Shule (*inapatikana shuleni*)
5) Ufagio Mrefu wa Chelewa (*Kufagilia uwanja*)
6) Brush ndogo za kusugulia sink (chooni)
7) Jembe 1 + mpini wake
8) Mopa na Ndoo yake
9) Hard broom (fagio ngumu)

**SARE ZA MICHEZO KWA SHULE**

- Track Suit za **BLUE** kwa Wavulana & Wasichana
- T – shirt za kuvalia Tracksuit (*ambazo zina Nembo ya shule*) zinapatikana shuleni
- Raba Nyeusi au Nyeupe za michezo kwa wote.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMUONDOA MWANAFUNZI BWENI

1. Kuchelewa kufika / kuripoti shuleni siku ya kufungua / kuanza shule au baada ya kumalizika kwa likizo ndefu / fupi.
2. Kuvunja sheria za shule.
3. Kuvaa nguo zisizo ruhusiwa kwa wakati unaotakiwa au kuvaa mavazi ambayo hayafuati maadili (nguo fupi na zinazobana au kaptura, n.k)
4. Kushindwa kuhudhuria masomo / maandalizi ya masomo wakati wa usiku kwa muda unaotakiwa na kusumbua wenzie kwa kupiga makelele au kulala badala ya kusoma.
5. Kushindwa kuungana na wenzie katika vipindi vya dini kabla ya masomo / maandalizi ya masomo ya usiku wakati wa kuanza na wakati wa kwenda kulala.
6. Kuanzisha vikundi / magenge yasiyo na mwelekeo wa kimasomo kama vile, kuvuta bangi, kucheza kamali, utoro wa vipindi darasani, Mizozo au kupigana / kupiga nk.
7. Kuiba mali za wenzie bwenini na kuharibu vifaa vya wanafunzi wengine kama vile, Nguo Matranka, Magodoro, nk.
8. Kusingizia kuumwa kusudi apate fursa ya kutokufanya mitihani au kurudi nyumbani.
9. Kushindwa kupata wastani wa alama za masomo unaokubalika kwa mwanafunzi wa BWENI.
10. Mwanafunzi kutohudhuria vipindi vya dini kwa mujibu wa ratiba.
11. Kuvuka Mipaka ya shule bila ruhusa ya Uongozi wa shule
12. Mzazi kutokuhudhuria vikao viwili mfululizo vya wazazi na ushiriki duni katika kupandisha taaluma ya mwanafunzi na shule kwa ujumla.
13. Kugomea Masomo, Mitihani, Chakula au wito halali wa shule.
14. Kutoka nje ya Bweni huku ukiwa umevaa mavazi kwa namna isiyozingatia maadili ya shule, kama vile Kifua wazi, Kuvaa mavazi mepesi yanayoonesha Maungo ya ndani ya mwili.
15. Kumuingiza mtu asiyestahili Bwenini kama vile, Mwanafunzi wa Kutwa, Mzazi/Mlezi, Au mtu mwingine yeyote.
16. Kuwa na vitu/vifaa visivyotakiwa Bwenini kama vile Visu, Mikasi, Vipodozi, Simu ya Mkononi, Earphone, Radio, Laptop, Line za Simu, Heleni, Cheni, Kacha, n.k.
17. Kumgomea Matron au Patron na Viongozi wa Bweni kwa jambo halali.
18. Uchafu wa mwili, nguo, na vyombo anavyotumia.

Mwisho mzazi unatakiwa kukiri kwamba unakubali masharti na taratibu hizi zote na upo tayari kukubali mwanao kuondolewa **BWENI** endapo masharti yamekiukwa na wewe mwenyewe au mtoto kama ilivyo elekezwa.

Pia unatakiwa kuhudhuria vikao vyote vya shule na vya wazazi wenye watoto BWENI. Hivyo kusaini kwako hapa inachukuliwa kwamba umekubaliana na sheria /taratibu zote za mwanao kukaa **BWENI**.

PICHA YA MZAZI/MLEZI

# TAMKO LA MZAZI / MLEZI

PICHA YA MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi / Mlezi wa (Jina la Mwanafunzi) na kidato ............................................................................................ Kidato cha........... mwaka 2025.

Ninakiri kwamba nimesoma na kuzielewa kanuni / taratibu na sheria za shule kwa ajili ya mwanangu awapo BWENI/SHULENI, hivyo nitakuwa tayari kukubaliana na maamuzi yoyote yatakayo chukuliwa na uongozi wa shule endapo mwanangu atakiuka kanuni/ taratibu na sheria zilizo ainishwa hapo juu.

Jina la Mzazi ..........................................................................................

Sahihi ya Mzazi ……………………………………………………….………………

Na. Simu (Mzazi /Mlezi) ……………………………………………………………